## 1.0 UTANGULIZI

Katika kutekeleza wajibu na majukumu yake, Jumuiya ya Wafanya biashara wenye viwanda na wakulima Zanzibar (ZNCCIA) imepewa mamlaka ya mshauri huru kufanya utafiti juu ya utawala wa kodi na mazingira ya biashara Zanzibar. Ushauri ulikuwa na lengo la kusoma sheria za kodi zilizopo Zanzibar ili kuja na mapendekezo ambayo yangewezesha kuleta mafanikio ya mfumo wa kisasa, wa haki na waushindani, ambao inaleta kufuata kodi na kuongeza ukuaji wa faida kwa sekta binafsi; na kwa njia hiyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kuzalisha ajira ndani ya visiwa.

Utafiti huo uliofanywa kwa kupitia sampuli ya walipa kodi 349 kutoka wilaya tano yaani Wilaya ya Mjini, na Magharibi Unguja na Mkoani, Chake Chake na wilaya Wete Pemba. Sampuli ilitayarishwa hasa ili kuvutia uwakilishi wa walipa kodi kwa makundi yote ya biashara (wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa). Uwakilishi pia uliakisi katika sekta za shughuli za biashara na mamlaka ya kodi ambapo sampuli ya walipa kodi wanalipa kodi zao.

Utafiti huu unatokana na imani ya ZNCCIA kwamba 'kuwa na mfumo wa kodi wa kisasa, rahisi, na wa haki na waushindani, ni njia muhimu ya serikali ya kujenga mazingira mazuri na kupunguza gharama za kufanya biashara'. Kufanya biashara katika mtazamo wa utafiti huu kunaweza kuelezwa kwa kiasi gani rahisi au vigumu kwa mwekezaji wa ndani Zanzibar kufungua na kuendesha biashara ndogo na za kati anapotekeleza kanuni husika kwa kuzingatia kwamba zaidi ya 90% ya wajasiriamali iko chini ya jamii ndogo na za kati.

Moja kati ya majukumu makubwa ya ZNCCIA, miongoni mwa mengine, ni utetezi. Kazi ya utetezi katika kufanya biashara inaweza kutazamwa katika muktadha mpana zaidi kulingana na nyanja kuu (kanuni) kwamba ni kuchukuliwa kuwa muhimu katika mzunguko wa maisha ya biashara. Utafiti huu unashughulikia hasa juu ya utetezi wa eneo la kulipa kodi. Utetezi unachukuliwa kama sehemu ya kusimamia mazungumzo na Serikali juu ya masuala ya maslahi ya umma.

## 2.0 SABABU YA UTAFITI JUU YA KUBORESHA UTAWALA WA KODI NA MAZINGIRA BIASHARA ZANZIBAR

Kama Jumuiya nyingine yoyote ya biashara, ZNCCIA in nia ya kuona kwamba kufanya biashara kunafanywa rahisi na mazingira ya biashara yanaimarika. Kodi inafanya moja ya masuala mpana katika mazingira ya biashara ambayo inachukuliwa kuwa ni kuzuia ukuaji na maendeleo ya biashara Zanzibar. Haina ufanisi kiutawala, na inaathiri vibaya ushindani wa sekta binafsi Zanzibar.

Utawala wa kodi katika Zanzibar una muundo wa ngazi tatu, yaani Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Utawala wa kodi wa Serikali za Mitaa. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inasimamia kodi zote zinazoanguka chini ya mambo muungano kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Bodi ya Mapato ya Zanzibar inasimamia kodi ya matumizi ya ndani ya Zanzibar, wakati Mamlaka za Mitaa zinasimamia kodi mbalimbali za mitaa chini ya usimamizi wa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kutokana na utata wa kiutawala katika mipango ya uhamasishaji wa rasilimali ndani ya Zanzibar, mfumo wa kodi ambao unatolewa pia umekuwa na utata. Hivyo, ili kukabiliana mahitaji ya kodi, walipa kodi Zanzibar wanakabiliana na mamlaka tatu tofauti. Utaratibu huu unasemewa, kwa kuongeza utata, pia kuongezeka kwa gharama za ufuatiliaji na gharama za utawala, kwa njia hiyo inaathiri katika ngazi ya hiari kufuata kulipa kodi na pia kuongezeka kwa gharama za kufanya biashara na kuathiri ukuaji wa uchumi.

Aidha, uundaji wa sera ya kodi Zanzibar iko chini ya mamlaka mbili, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) Bunge kwa ajili ya kodi ya Muungano kwa mujibu wa sehemu ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa upande mmoja, na Baraza la Wawakilishi kwa taasisi ambazo si za muungano, kwa upande mwingine. Wadau kwa upande wa Zanzibar wanahisi kwamba sera ya kodi yenye ufanisi Zanzibar inapaswa kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kuweka utawala ambao unaunganisha na sekta kiongozi, yaani biashara na utalii. Kwa ujumla, utalii haujaunganishwa na sekta nyingine za uchumi wa Zanzibar.

Kwa upande wa sera ya kodi, mageuzi kadhaa yamefanyika ikiwa ni pamoja na kumalizwa kero ya kodi, kuoanisha mfumo wa udhibiti, utoaji wa motisha wa kodi, kupunguza viwango, kupanua wigo wa kodi na jumla ya usawazishaji wa sera ya kodi. Licha ya mageuzi, bado kuna baadhi ya vikwazo katika urahisi wa kufanya biashara. Ufanisi wa hatua za usajili na tathmini kwa walipa kodi zinaonesha kwamba hakuna uhusiano kati ya mtandao wa usajili (database) ya ZRB na TRA hivyo hali hiyo inaleta hali ya kutokua na usawa katika uwekaji wa adhabu kati ya mamlaka ya kodi mbili.

## 3.0 MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo makuu  ya utafiti ni pamoja na yafuatayo:

### 3.1 UTAWALA  WA KODI

Utoshelevu wa Mapato

Kulingana na jumla ya mapato yaliyokusanywa na jumla matumizi, uwezo wa nchi ili kukidhi mahitaji yake ya bajeti ilikuwa 55.7% ya mahitaji yote.

Sababu ya upungufu wa mapato ya fedha ilikuwa inatokana na sababu kama vile utegemezi juu ya sekta moja kubwa na na ambayo ina udhibiti mzuri wa kodi (sekta ya huduma) na ari ndogo kodi, miongoni mwa nyengine. Sababu za kitaasisi ikiwa ni pamoja na mfumo wa kisheria pia umeonekana unaathiri mapato chini ya kiwango.

**Ari ya Walipa kodi**

Utafiti umebaini kuwa 74.3 ya walipa kodi wa makundi yote hawakuwa na ari ya kulipa kodi. Sababu kuu zilikuwa: hawaamini

kwamba Serikali inatumia fedha za walipa kodi kwa busara na / au kutumia kwenye bidhaa za umma ambazo zinawanufaisha walipa kodi na mtazamo kwamba kodi ya serikali si haki kwa maana ya kwamba baadhi ya walipa kodi walikuwa hawalipi kodi.

**Madhara ya ufanisi wa Kiuchumi**

Kuwepo kwa mifumo miwili ya fedha kwa biashara ndogo ndogo kunaleta kuanguka kwa uchumi wa Zanzibar kwa sababu:

Mwingiliano wa sheria ya kodi kwa msingi ule ule ambao unaleta mzigo nzito wa kodi kwa walipa kodi wa Zanzibar ikilinganishwa na Tanzania Bara; hivyo uwezo wa biashara ndogo ndogo kukua kwa njia ya kujiwekea akiba ni mdogo na kwa wale ambao waliopata mikopo midogo midogo walikuwa wanashindwa kulipa mikopo yao.

Juhudi za Serikali kuelekea kupunguza umaskini wa kipato kupitia sera ujasiriamali unahatarishwa na Taasisi za Mikopo zinakabiliwa na madeni mbaya kwavile biashara ndogo ndogo hazina dhamana ya usalama kwa kiwango kikubwa

**Madhara ya Huduma za kulipia kodi juu ya Kukuza Uchumi**

Elimu duni za walipa kodi na utoaji huduma usiokamilika ulilalamikiwa na watu wengi waliohojiwa na utafiti huu kama moja ya sababu kubwa za kutofuata taratibu za kulipa kodi Zanzibar.

Karibu nusu ya walipa kodi (49.9%) walikuwa na maoni hasi juu ya athari za utoaji wa huduma za walipa kodi juu ya kuchochea ukuaji wa biashara. Kwa upande mwingine wastani wa 39.2% walionesha maoni chanya na 10.9% walikuwa si wenye ujuzi juu ya suala linalozungumzwa.

**Wajibu Mwafaka Walipa kodi**

Utafiti uligundua kuwa walipa kodi walikuwa hawana furaha juu ya mamlaka ya kodi jinsi ya haki zao zinavyoshughulikiwa na wengine hawajui haki zao. Hii ina maana kwamba uhamasishaji juu ya haki za walipa kodi na wajibu ni ama unakosekana au si waufanisi.

Theluthi mbili (67.6%) ya washiriki walikuwa na mtazamo hasi juu ya sababu zinazochangia kufuata matakwa ya kulipa kodi kwa hiari.

Kwa upande mwingine, 21.3% walikuwa na mtazamo chanya, wakati 11.1% hawafahamu juu ya suala lenyewe licha ya kuwa katika shughuli za biashara kwa miaka mingi.

**Haki na Wajibu wa mlipa kodi**

Karibu robo tatu ya walipa kodi (73.8%) hawafurahishwi na jinsi ya mamlaka ya kodi inavyo shughulikia haki zao. Baya zaidi kiasi cha 13.0% ya walipa kodi hawakuwa na ufahamu wa haki zao ikimaanisha kwamba uhamasishaji walipa kodi juu ya haki za walipa kodi na wajibu ni ama haupo au haunaufanisi.

Utafiti uligundua kwamba haki na wajibu za walipa kodi hazikufafanuliwa wazi katika nyaraka za Serikali za Mitaa.

Kiasi ya 70% ya waliojibu walieleza kwamba haki na wajibu wa mlipa kodi hazikufafanuliwa wazi katika nyaraka za Serikali za Mitaa; na kiasi ya 13% baadhi yao hawakuwa na wazo lolote juu ya haki za walipa kodi na majukumu yao licha ya kuwemo katika biashara kwa kwa muda mrefu.

**Matumizi ya ICT katika usimamizi wa mapato**

Matokeo yalionesha kuwa nusu ya waliojibu walikuwa na maoni kwamba matumizi ICT yalikuwa athari chanya katika usimamizi wa kodi. Nusu iliyobaki walikuwa na maoni tofauti ama kwa kuamini kwamba kulikuwa hakuna kuongeza ufanisi au kuwa hawajui athari hata kidogo.

**Utawala wa Forodha**

Chini ya nusu ya walipa kodi walikubaliana kwamba mipango ya kisasa imeleta matunda na malengo yake yamepatikana. Wakati kiasi cha 28.0% hawakukubaliana na, kiasi ya 25.0% walijibu kuwa hawana taaluma juu ya nini kinachoendelea baada ya programme kuanza.

**Utekelezaji wa Kodi**

Utekelezaji wa Kodi unawakilisha tatizo kubwa kwa mifumo ya kodi Zanzibar kwa sababu hawana rasilimali au ujuzi wa kujua jinsi ya kugundua udanganyifu, ukwepaji kodi au masuala magumu ya kodi.

Ukosefu wa utaalamu juu ya mbinu za kisasa na vifaa vinavyotumiwa na wanaokiuka zilikuwa ni miongoni mwa sababu za utawala za kodi Zanzibar kuwa hauwezi kupata picha halisi ya shughuli za biashara ya walipa kodi. Suala la tofauti ya kiwango cha teknolojia kati ya walipa kodi (mfano makampuni ya kimataifa) na utawala wa kodi ina jukumu kubwa pia.

**Leseni ya Biashara**

Utafiti huu umebaini kuwa utoaji was leseni ya biashara Zanzibar ni kero kwa walipa kodi. Baadhi ya taasisi za Serikali zinatoa leseni kama sharti kwa ajili ya kufanya biashara katika maeneo yao ya mamlaka. Vile vile, utoaji wa leseni unahusisha taasisi wadau nyingi na kila moja inaweka ada za leseni. Dhamira ni mapato na sio kufanya kazi kama taasisi ya udhibiti. Kutokana na suala hili, mlipa kodi ili aweze kufanya biashara ni lazima aambatane na mfululizo wa malipo wa katika hali ya ada za leseni achilia malipo mengine ya lazima yanayolipwa kwa Serikali.

Imebainika pia kwamba ZRB, wakala pekee kwa ajili ya kukusanya mapato ya ndani kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inakusanya kodi ya leseni ya biashara badala ya kuwa Mamlaka ya Leseni (Biashara Msajili). Leseni ya biashara katika hali kama hiyo ni kweli kwamba inatumika kama chanzo cha mapato kinyume na desturi ilivyo duniani kote.

## 3.2 SERA YA KODI

### Uwazi na urahisi wa Sheria ya Kodi

Sheria ya kodi katika ya Zanzibar ni ngumu na inatoa mwanya kwa ukwepaji au uzuiyaji

kodi. Hawana urafiki kwa walipa kodi ambao wana elimu ndogo ya kisheria na hivyo kutolipa kodi kunachangiwa na utata wa utawala wa kodi wa sasa.

Kiasi ya 73% ya walipa kodi walikuwa na maoni kwamba sheria ya kodi haziko wazi, ni ngumu mno na hivyo si rahisi kueleweka hususan kwa wafanya biashara ndogo ndogo na za kati.

Utafiti umebaini baadhi ya maafisa wa kodi hususan kwa Serikali za Mitaa hawana uwezo wa kutosha juu ya masuala ya kodi. Kadhalika kwa wafanyakazi wa TRA na ZRB kuna haja ya kuwa na utaalamu katika baadhi ya sekta kwa mfano huduma za fedha, mawasiliano ya simu, ujenzi na utalii (kwa sababu ya utalii wa bahasha) kwa ajili ya ukusanyaji bora wa mapato kutoka sekta hizi.

Kiasi ya 80% ya waliohaojiwa hawakuwa na taaluma na maarifa juu ya masuala ya kodi

**Wepesi na Haki ya Mfumo wa Kodi**

Utafiti umebaini kuwa 85% ya waliohojiwa walikuwa na maoni kwamba viwango vya kodi si vya haki kwa maana ya kwamba viko juu kiasi.

Mpango wa uundaji wa sera Zanzibar unaonekana kama kizuizi kwa mafanikio ya biashara kutokana na ubaguzi wake katika mfumo wa motisha kwa baadhi ya walipa kodi kitu ambacho kimesababisha mzigo kwa jamii na ukuaji mdogo wa biashara.

Kiasi ya 78% ya waliojibu hawakukubaliana kwamba hakuna ubaguzi katika kodi ya uundaji wa sera.

**Utawala wa Misamaha ya Kodi**

Sheria ya uwekezaji Zanzibar inatoa faida kubwa ya msamaha wa kodi katika maeneo ambayo yamefunguliwa kwa DFIs (Uwekezaji ya Nje wa moja kwa moja) na uwekezaji wa kitaifa wa sekta binafsi. Hizi ni pamoja na huduma za Fedha na biashara, ikiwa ni pamoja na bandari na bandari huru kwa ajili ya kituo cha shughuli za Utalii;, viwanda hasa na mwelekeo wa nje; makao makuu ya kikanda kwa ajili ya huduma za fedha na biashara; sekta ndogo ya Samaki na bahari; na Biashara. Hata hivyo imebainika kwamba 'Kupungua viwango vya kodi na motisha inaweza kuvutia uwekezaji wa ndani na nje lakini tu ambapo hali nyengine za biashara ni nzuri. Tafiti za kibiashara kwakurudia zimegundua kwamba wakati masuala kodi kwa wawekezaji, hali nyingine kama miundombinu, utawala wa sheria, na ubora wa gharama za wafanyakazi zaidi una umuhimu zaidi. (McKinsey, 2003, Van Parys na James 2009 na Dharmapala na Hines, 2009).

Kiasi ya 57% ya waliojibu walionesha kuwa misamaha ya kodi imekuwa ndio chanzo cha matatizo katika nyanja nyingi za sera ya fedha kama vile - ukwepaji wa kodi, mmomonyoko wa kodi msingi, ubaguzi wa kodi, nk, Pia wanaamini kwamba hakuna haja ya msamaha wa kodi kwavile wao ni wakarimu na wanabaguliwa katika asili.

**Mageuzi ya Sera ya Kodi**

Kiasi ya 82% waliamini kuwa ushiriki wa sekta binafsi katika sera ya kodi unaweza kusababisha makubaliano kati ya sekta

binafsi na ya umma kwa ajili ya kuboresha utawala wa kodi na ukuaji wa biashara.

Vile vile, 82% waliamini kwamba ushiriki wa ufanisi wa wanachama wa Zanzibar katika kikundi cha kazi ya mageuzi ya kodi ya muungano ingeweza kupunguza masuala yenye utata juu ya kodi ya Muungano na yale yanayosimamiwa na ZRB.

**Kuunganisha Walipa kodi katika wavu kodi**

Kiasi ya 65% ya waliojibu walikubaliana juu ya hatua ya kuwaingiza katika wavu kodi ya wale walipa kodi ambao huzalisha kiasi kidogo cha mapato kulingana na ajenda ya mageuzi ya kodi ya kupanua wavu kodi kupitia:

- Kuanzishwa kwa vituo vya ukusanyaji vinavyotembea, elimu ya walipa kodi na programu za uhamasishaji na ushirikiano kati ya mamlaka ya kodi na sekta isiyo rasmi/jumuiya za microenterprise,
- Kuanzishwa kwa mfumo maalum wa usimamizi kwa mamlaka zote za kodi ikiwa ni pamoja na kushirikiana na mamlaka za mitaa, na
- Hatua ya Serikali ya kuimarisha utekelezaji wa waendeshaji sekta isiyo rasmi kwa njia ya elimu na mipango ya kuwafikia, ikiwa ni pamoja na msamaha wa biashara ndogo.

**Mlolongo/Utitiri wa Kodi**

Suala la kodi nyingi limeonekana kama jambo kubwa kwa karibu ya wote waliohojiwa katika utafiti huu. Mfano wa kawaida hapa ni sekta ya utalii ambayo ina mlolongo wa kodi / ushuru / ada. Hali hii kwa kweli kwa vigezo vyovyote vya kiuchumi si nzuri kwa ukuaji wa biashara na ingeweza kusababisha mazingira ya machafuko na madhara katika jamii ya walipa kodi. Kampuni ya kawaida katika sekta ya utalii Zanzibar inalazimika kulipa kodi kiasi ya aina 10.

## 4.0 UCHAMBUZI WA KULINGANISHA ZANZIBAR NA CHUMI ZA VISIWA VYINGINE VIDOGO

### 4.1 UCHAMBUZI KULINGANISHA NA URAHISI WA KULIPA KODI

Wastani wa jumla ya kiwango cha kodi katika uchumi wa kisiwa kidogo ni 37.2%, ikilinganishwa na wastani wa kimataifa wa 48.3%. Takwimu zinaonesha kwamba Maldives ilikuwa katika nafasi ya kwanza Taifa la Kisiwa kwa urahisi wa kulipa kodi mwaka 2010. Ilikuwa ikifuatiwa na Singapore, Mauritius kwa safu ya 4 na 12. Wawili wa mwisho walikuwa Jamaica na Belarus wakiwa ni 178 na 203 kuonesha kwamba walikuwa na Uchumi wa Kisiwa ulio mgumu katika urahisi wa kulipa kodi.

Zanzibar ilikuwa katika nafasi ya 103 katika urahisi wa kulipa kodi ambapo ulikuwa ni bora ya zaidi ya Dar es Salaam na alama ya wastani ya Sub-Sahara Afrika ilikuwa na nafasi ya 120 na 112 kwa mtiririko huo lakini ilikuwa mbaya zaidi ikilinganishwa na

wastani wa alama ya Uchumi wa Kisiwa kidogo(67). Takwimu katika kwa kulinganisha na idadi malipo ya kodi kwa mwaka, Zanzibar inaoana na Dar es Salaam kwa malipo ya 48 na ilikuwa ni mbaya zaidi ikilinganishwa na wastani wa alama ya malipo ya 28 na 38 kwa malipo ya Uchumi wa Visiwa Vidogo na Afrika Kusini mwa Sahara kwa mtiririko huo. Kwa muda uliotumika katika mchakato wa kulipa kodi, kampuni ya kiasi cha kati Zanzibar huchukua masaa 158 kinyume na masaa 172 kwa Dar es Salaam, masaa 160 kwa uchumi wa kisiwa na masaa 306 kwa Afrika Kusini mwa Sahara. Katika suala hili la wakati unaotumika kwa ajili ya malipo ya kodi, Zanzibar ni nzuri ikilinganishwa na nchi nyingine za kusini mwa Sahara Afrik

Katika kisiwa cha Maldives, mfano wa kampuni ya kiwango cha kati inatanya malipo mara moja, inalipa 9.1% ya faida yake ya kibiashara katika kodi, na i chini ya saa moja kwa mwaka kwa kulipa kodi. Hii ilikuwa utendaji bora wa kimataifa katika kulipa kodi mwak Ambapo katika mji wa Zanzibar, kampuni yenye ukubwa wa unaofanan i malipo 48, inalipa 40.8% ya faida yake ya kibiashara katika kodi, na inatumia 158 kwa mwaka katika kulipa kodi hali kama hii, unaweza kuona jinsi gani ilivyo vigumu kwa walipa kodi ku biashara Zanzibar.

## 4.2 UCHAMBUZI LINGANISHI KATI YA ZANZIBAR NA MAURITIUS

Zanzibar kieneo ni kubwa kuliko Mauritius, lakini kwa idadi ya watu wao n ukilinganisha na Zanzibar. Katika nyanja za kiuchumi, nchi hizi mbili ziko mbali mbali ambapo Zanzibar imewekwa kwenye kundi la nchi zenye maendeleo ya chini wakati Mauritius ni moja ya nchi zenye kipato cha kati, na wastani wa mapato ya kila mwaka kwa kila mwananchi ambayo ni mara 14 kubwa kuliko Zanzibar. Uchumi wa Mauritius una uwezo wa kuhimili kodi zaidi unao ungwa mkono na uchumi wenye nguvu kama nchi ya kipato cha kati ambayo inafurahia sana maendeleo ya ICT. Muhtasari wa viashiria kwa ajili ya kulinganisha imetolewa katika Jedwali 1.

**Jedwali 1: Viashiria vywa kulinganisha**

| S/N | Indicator | Zanzibar | Mauritius |
|---|---|---|---|
| **1** | Area (Sq.kms) | 2,654 | 1,860 |
| **2** | Population (million) | 1.2 | 1.3 |
| **3** | Per-capita GDP (US$) | 561 | 7990 |
| **4** | ***Sector Contribution to GDP (%)*** | | |
| | Agriculture | 32.8 | 4.9 |
| | Industry | 12.6 | 23.1 |
| | Services | 42.5 | 72 |
| **5** | ***Tax Rates (%)*** | | |
| | VAT rate | 18 | 15 |
| | Corporate tax rate | 30 | 15 |
| | Individual income tax rates | 15, 20, 25 & 30 | 15 |
| | Annual Revenue growth (%) | 3.7-26.6 | 15-20 |
| | VAT Threshold (US$) | 19,056 | 68, 236 |
| **6** | **Revenue as % of GDP:** | | |
| | **Total Domestic Revenue** | **16.4** | **21.0** |
| | **Tax Revenues** | **15.4** | **19.0** |
| | Import Duty | 1.6 | 0.6 |
| | Excise Duty | 0.6 | 3.6 |
| | Value Added Tax | 5.9 | 8.1 |
| | Income Taxes | 2.1 | 5.4 |
| | Corporate | 0.5 | 3.3 |
| | Personal | 1.3 | 1.7 |
| | Other Income | 0.2 | 0.4 |
| | Other Taxes | 5.1 | 1.3 |
| | **Non-Tax** | **1.0** | **2.0** |
| **7** | Exemption as % of GDP | 8.2 to 7.6* | 3.2 to 1.5 |

## 5.0 MAPENDEKEZO

### 5.1 KWA UJUMLA

**Kujenga Utamaduni wa kulipakodi**

- Serikali inapaswa kuchukua hatua za makusudi kujenga utamaduni wa walipa kodi, hasa kwa kuongeza mapato ya ndani na kukuza usawa na haki katika mfumo wa kodi. Utamaduni wa kulipakodi ni kutia moyo walipa kodi kwa njia ya elimu kwa walipa kodi na kuwa na mashirikiano ya kiubunifu kati ya serikali na wananchi juu ya masuala ya kodi.

- *Kumbuka: maeneo matatu muhimu yanayofungamana kwa kujenga utamaduni wa walipa kodi na kuimarisha kufuata kodi ni sera ya kodi, utawala wa kodi na hatua za nje ya mfumo wa kodi (ikiwa ni pamoja na jinsi ya mapato ya kodi yanavyoitumika na kwa kiwango gani kodi inahamasisha ushiriki wa wananchi kisiasa. Hivyo,. haja ya kuimarisha upande wa mahitaji ya uwajibikaji wa kodi, yaani kuhamasisha ushiriki mpana raia katika kodi. Jukumu la vyombo vya habari, vyama vya kiraia, Bunge / Baraza la Wawakilishi na mashirika mengine ya usimamizi wa kitaasisi ni muhimu katika suala hili.).*

- Ili kujenga utamaduni wa ufanisi kwa walipa kodi viongozi wa kodi lazima wajenge uhusiano mzuri na walipa kodi badala ya uhusiano wa kipolisi na mkosaji ambao umepitishwa na baadhi ya maafisa wa kodi kwa sasa.

- Ingawa jukwaa la walipa kodi Zanzibar limeanziswa, inapendekezwa kwamba wawakilishi wa jamii wanapaswa kushirikishwa katika kila ngazi maamuzi juu ya masuala yanayohusu kodi ili kuvuta ukuaji na mageuzi ya ufuataji wa kodi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali .

- Kwavile kikundi kazi kwa ajili ya ushirikishwaji wa mageuzi ya kodi hakipo kisheria, inapendekezwa kwamba uundaji wa kazi lazima kuhalalishwa na kubainisha idadi ya ushiriki wa sekta binafsi katika kikundi kazi hicho pamoja na ngazi ya kuhusika katika utoaji wa maamuzi wa sera ya kodi.

- Aidha, inapendekezwa kwamba Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha wawakilishi wa sekta binafsi katika bajeti matumizi ya umma ili kujenga imani miongoni mwa wananchi juu ya njia ambayo fedha za walipa kodi zinatumika kwa ajili ya maendeleo ya kitaifa.

**Utekelezaji wa Bandari Huru (Freeport)**

Katika ari ya kukuza biashara, Tanzania inaweza kuchagua kutekeleza Sehemu G ya Ibara ya 31 ya Itifaki ya Kuanzishwa kwa

Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutambua Zanzibar kama ukanda maalum wa kiuchumi pamoja na uanzishwaji wa Bandari Huru. Hakika rasimu ya sera ya biashara Zanzibar inalenga kwamba.

Wazo la bandari ya huru Zanzibar sio geni. Kwa kweli bandari ya huru tayari ipo kupitia Mamlaka ya Bandari Huru Zanzibar iliyoanzishwa na Mamlaka ya Bandari Huru Zanzibar Na.9 ya 1998. Sheria ilianza kazi Agosti 2000 kama sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuendeleza biashara na huduma nyengine. Lengo kuu la kuanzisha ZFPA ni kuutawanya uchumi wa Zanzibar na kuharakisha maendeleo ya visiwani. Hivyo, ni wakati muafaka kwamba Serikali iweze kutekeleza rasmi bandari ya huru Zanzibar ili kufufua uchumi wake.

## 5.2 KODI UTAWALA

### (i) Huduma ya Elimu ya kulipia kodi

- Tawala za kodi lazima kubuni utaratibu wa kuboresha mwamko kwa walipa kodi katika masuala ya kodi ikiwa ni pamoja na uelewa wa sheria ya kodi, haki za walipa kodi na mageuzi ya majukumu ya fedha yanayopitishwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ili kuboresha kufuata kodi kwa hiari.
- Jumuiya ya walipa kodi inapaswa kuwa na jukumu muhimu katika kuongeza uelewa juu ya majukumu ya walipa kodi huku wakifurahia haki zao ili kujenga hali ya kukubaliana (*win-win situation*) kati ya jumuiya ya walipa kodi na Serikali.
- Utawala wa kodi unatakiwa kuwekeza zaidi katika ICT ili kuongeza matumizi ya ufanisi ya ICT katika utawala wa kodi.

### (ii) Ari kwa walipa kodi

- Serikali inapaswa kuzingatia sheria ya usimamizi wa fedha za umma na kanuni na kutumia fedha za walipa kodi kwa busara katika maeneo ambayo yanavutia maslahi ya umma ili kuongeza ari ya walipa kodi ya kulipa kodi.

**(i) Sababu za Kukataliwa Usajili wa VAT**

- Ili kupunguza malalamiko ya walipa kodi, inapendekezwa kwamba TAPA No 2009 kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha pamoja maelezo ya sababu za kukataliwa usajili wa VAT.

**(ii) Uadilifu wa Watumishi**

- Unyanyasaji unaofanywa na maafisa wa kodi au na ushirikiano kati ya walipa kodi na viongozi wa kodi ambao unashawishi rushwa kwa kweli ni tatizo katika tawala za kodi, hivyo

tunapendekeza kwa Serikali yafuatayo:

- Kuanzisha kamati za maadili kwa wafanyakazi katika ngazi mbalimbali za utawala wa kodi kwa lengo la kupambana na tabia zinazokwenda kinyume na maadili mema kwa wafanyakazi ambazo husababisha hasara ya mapato.

- Kuanzisha Fomu za Azimio Mali ambazo hujazwa na wafanyakazi kwa kila mwaka. Kwa ajili ya kutekeleza pendekezo hili, Serikali inaweza kufikiria kuanzisha kitengo cha Mambo ya Ndani katika kila taasisi ya kodi.

- Kwa ajili ya uwazi na kujenga nguvu ya uaminifu ya umma kati ya mamlaka ya kodi na jumii ya walipa kodi, inapendekezwa pia kamati za maadili ya wafanyakazi lazima kuchukua wanachama kutoka kwa umma ikiwa ni pamoja na vyombo viwakilishi vya walipa kodi.

- Uundaji wa kamati na kanuni za adhabu inapaswa kwenda sambamba na kanuni za maadili ya wafanyakazi ya taasisi za kodi na ofisi ya taifa ya iliyo na wajibu wa kupambana na vitendo vya rushwa katika Zanzibar.

**Leseni ya Biashara**

Ni wakati muafaka kwamba Serikali iweze kufikiria njia bora ya kutoa leseni za biashara kwa njia ya kuteua / kuanzisha taasisi moja kama shirika la udhibiti litalowajibika na kutoa leseni ili kuzuia taasisi nyingine za kutoa leseni kwa madhumuni ya mapato.

## 5.3 SERA YA KODI

### (i) Kufanya utafiti wa kina

Ili kupunguza malalamiko ya sera ya kodi, Serikali inapaswa kujiegemeza kwenye utafiti wa kina ambao utatanda karibu masuala yote ya fedha na sera zinazohusiana ili kujenga utawala wa kodi wa kisasa kwa lengo la:

- *Kurahisisha utawala wa kodi* ambao ni huru kutokana utawala mgumu, ambao hauna nguvu nyingi za hiari na motisha ya kodi ambayo haina faida kiuchumi. Kurahisisha lazima pia ilenge katika kuondoa fursa kwa ukwepaji kodi na kuepusha kutokana na mfumo tata wa kodi na usio wa uwazi;

- Kupanua na kuimarisha wigo wa kodi

- Kuondoa ubaguzi na kuboresha usawa katika mfumo wa kodi kwa njia ya kurahisisha utawala wa motisha wa kodi na kupunguza migogoro ya kisheria kati ya taasisi zinazosimamia utawala wa motisha wa kodi.

- Kupunguza gharama ya walipa kodi kwa ajili ya uboreshaji wa walipa kodi kwa hiari,

- Kusawazisha muundo wa kodi sambamba na utekelezaji bora kwa kubaki na kodi chache.

- Kuanzisha sera ya matumizi ya kodi kwa ajili ya kuboresha usimamizi wa matumizi ya bajeti ya Serikali kwa kufanya matumizi ya kodi kama sehemu ya bajeti kama ilivyokuwa kwa Brazil na Peru ili kuongeza uwazi wa fedha.

- Kurahisisha usimamizi wa mapato kwa kuanzisha mfumo mmoja wa kodi ya serikali ambao unashajiisha kuoanisha kodi katika viwango vinavyongoza.

**(ii) Utozaji Kodi Sekta isiyo rasmi**

Kwa kutumia mpango uliopo, inapendekezwa kufanya yafuatayo:

- Andaa baadhi ya utunzaji kumbukumbu wa msingi (uliorahisishwa) na hivyo kufanya ni lazima kwa walipa kodi wote wadogo kuweka baadhi ya fomu za kumbukumbu za msingi za biashara au nyaraka zinazoonesha mauzo na baadhi ya gharama kwa kupitia mifano maalum inayotolewa na TRA. Kumbukumbu zinaweza kupunguzwa zikawa ni muhtasari tu kama risiti au malipo ya kila wiki, kila siku au kila mwezi;

- Unganisha kodi ya biashara ndogo na faida zinazoonekana wazi, hasa zaidi kuunganisha na baadhi ya faida za kijamii, kama katika uhusiano na Mamlaka ya Udhibiti Usalama wa Jamii (Social Security Regulation Authority) na mfuko wa hifadhi ya jamii kuendeleza taratibu ambapo sekta isiyo rasmi wamesajiliwa katika mamlaka ya kodi inaweza kujiunga na mipango ya hifadhi ya kijamii na michango ya robo mwaka au kila mwaka kwa kupitia mfumo wa kodi. Brazil sasa hivi inatekeleza mbinu hii.

- Aidha, inapendekezwa kutumia mbinu zifuatazo kwa ajili ya kuunganisha biashara ndogo ndogo katika wavu kodi na kurahisisha usajili na kuleta zaidi *non-filers* na wasiolipa kodi katika wavu.

- Kuanzishwa vituo mwendo vya ukusanyaji, elimu ya walipa kodi na programu za uhamasishaji na ushirikiano kati ya mamlaka ya kodi na sekta isiyo rasmi/ wajasiriamali wadogo.

- Kuanzishwa kwa mfumo maalum wa usimamizi kwa mamlaka zote za kodi kwa kuwekwa pamoja kwa kushirikiana na serikali za mitaa.

- Hatua za Serikali za kuimarisha utekelezaji wa waendeshaji sekta isiyo rasmi kwa njia ya elimu na

mipango ya kuwafikia, ikiwa ni pamoja na msamaha wa biashara ndogo.

- Kodi ya muda ya SMEs lazima kuanza kulipwa katika maadhimisho ya mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa biashara. Hii ingekuwa kuashiria kwamba katika usajili wa kodi hakuna muda iliyokusanywa, kwa vile biashara itakuwa haina mapato wakati ule.

**(iii) Muundo wa Kiwango cha Kodi**

**PAYE**

- Ili kupunguza mzigo wa walipa kodi sambamba na MKUZA Nguzo ya Kwanza (Kukuza Uchumi na Kupunguza umaskini, kuna haja ya kuunganisha muundo wa PAYE uliopo pamoja na wa Bara kwa kupunguza kiwango cha chini kutoka 15% hadi 14%.

**Tozo la Ujuzi na Maendeleo**

- Ili kupunguza tatizo la asili liliomo katika SDL yaani la kuondosha motisha kwa ajira na kupunguza uwezekano wa mishahara bora, inapendekezwa kwamba muda wa kati kuwekwa kwenye 2% ili kupata utendaji bora.

**Ongezeko la Thamani (VAT)**

**Kizingiti cha VAT**

- Katika suala la kizingiti, Zanzibar ina baadhi ya wigo wa kuongeza au kurejesha hiyo kwa kiwango cha sasa. Lakini kwa ajili ya kupunguza gharama za utendaji na kwenda sambamba na wastani wa kiwango cha Afrika Kusini mwa Sahara / au nchi wanachama, inapendekezwa kuongeza kizingiti hatua kwa hatua chini ya mipango ya muda wa kati.

**Kiwango cha VAT**

- Kuna hali ya kutiwa nguvu katika baadhi ya kupunguza kiwango cha VAT bila ya kuwa na mapato ya kifedha yaliyo madhubuti. Katika suala hilo, 17% au 16% Zanzibar bado watakuwa na kiwango cha kulinganishwa na nchi nyingine katika Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, na inaweza kuwa na uwezo wa kuendeleza Mapungufu yanayotokana humo. Kama kiwango cha kufuata kitaongeza kila muda, sadaka ya fedha itapunguzwa moja kwa moja. Kwahivyo ilipendekezwa kwa Serikali kupunguza VAT hatua kwa hatua kwa kiwango cha asilimia 16.

**Usajili wa VAT kwa wasafirishaji bidhaa**

- Ili kupunguza malalamiko ya walipa kodi, inapendekezwa kwamba, sababu za VAT kukataa kusajili lazima zifafanuliwe wazi kwenye TAPA kama ilivyokuwa kwa sehemu ya 6 (2) (a) hadi (e) ambayo inaeleza mahitaji kwa ajili ya usajili wa VAT.

**Ushuru wa stempu kwenye biashara ndogo ndogo**

- Ili kupunguza mzigo na wakati huo huo kuwa na utekelezaji wa ufanisi wa MKUZA Nguzo ya Kwanza, Serikali inaweza kufikiria kufuta ushuru wa stempu na badala yake kutekeleza mfumo rahisi wa kodi ya mapato kwa ajili ya biashara ndogo ndogo.

**Tozo la Hoteli, Mikahawa na Waongozaji Wageni**

- Kimsingi, kodi hizi zinatozwa kwa huduma zinazotolewa na kundi lile lile la walipa kodo, hivyo ili kuufanya mfumo wa kodi uwe ni wenye haki, inapendekezwa kubuni kodi moja (kwa jina lolote litakaloitwa) itozwe kwa msingi huo badala ya kodi tatu zilizopo sasa hivi.

- Aidha, inapendekezwa kwamba Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kubadilisha njia ya kuwalipisha kodi watembezaji wageni / huduma za hoteli kulingana na viwango vya fedha za utalii ambazo wanatozwa watalii na sio kwa ile ya mapato yanayo tozwa na mamlaka.

**Kodi ya Mafuta ya petroli**

- Kutokana na umuhimu wa bidhaa za mafuta katika michakato ya uzalishaji na usambazaji. Inapendekezwa kwa Serikali kupunguza mzigo wa kodi kwa bidhaa hizo kwa kuzingatia Kuunganisha tozo la Petroli na Mfuko wa Maendeleo ya Barabara.

## 6.0 HITIMISHO

Kuwepo kwa mfumo mamlaka tatu Zanzibar kumechangia kuwepo na malalamiko zaidi ya walipa kodi, ari ya chini ya kulipa kodi kwa walipa kodi na hivyo kiwango kidogo cha kukubali kodi.

Maoni ya wadau juu ya kuanzishwa sera ya kodi yenye ufanisi Zanzibar ili kukuza uchumi kwa kuweka mamlaka ambayo itaunganishwa na sekta viongozi kwa ukuaji wa uchumi, yaani biashara na utalii ni halali na ipewe kipaumbele. Sekta ya utalii kwa hali ya mambo ilivyo sasa haikuunganishwa na sekta nyingine za uchumi wa Zanzibar.

Kama hatua ya kujenga utamaduni wa walipa kodi, ushiriki wa sekta binafsi katika chombo cha maamuzi ya sera ya kodi ni lazima.

Jitihada za kupanua wigo wa kodi kwa undani unashikamana na ubora wa matumizi ya serikali. Ikiwa mlipa kodi anahisi kuwa malipo ya kodi hayatumiki ipasavyo au yanapotea, hali ya kukubali kodi itkuwa ni ya chini na mageuzi ya kodi yatakuwa mbali chini ya ufanisi (Fielstad na Heggstad).

Changamoto kwa ajili ya utawala bora wa mapato Zanzibar ni ukosefu wa huduma bora za walipa kodi na maarifa ya kushawishi ukubalifu wa hiari kwa walipa kodi.

**Kwa madhumuni ya kuwa na Chombo/Mamlaka ki/moja cha Kodi**, pendekezo la kufanya utafiti wa kina ili kuja na mageuzi ambayo yatabadilisha utawala wa sasa wa kodi kuelekea na mfumo mmoja wenye ufanisi zaidi ni wakati hasa na lazima kuchukuliwa kama mpango wa kipaumbele kuelekea kupunguza matatizo kodi yaliyopo.